

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
TANGAZO KWA UMMA

TAARIFA KWA WAMILIKI WA RASILIMALI ZINAZOTOZWA ADA NA TOZO KWA MWAKA 2022/2023

Kwa taarifa hii, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, linawakumbusha wamiliki wa miradi na shughuli nyingine zilizotajwa katika Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Ada na Tozo) za mwaka 2021 (Tangazo la Serikali Na. 387/2021), kwamba wanatakiwa kulipa Ada na Tozo stahiki za mwaka 2022/2023 kabla ya tarehe 30 Desemba, 2022.

Aidha, wamiliki wa miradi na shughuli husika wanatakiwa kuzingatia kuwa, ada na tozo za mwaka zitakazolipwa baada ya tarehe hiyo, watatozwa adhabu ya asilimia tano (5%) kwa mwezi na wanaweza kushitakiwa kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na ulipaji wa Ada na Tozo, Baraza linawataka wamiliki wa miradi na shughuli zilizotajwa katika Kanuni ya 2021, kuwasilisha kwa maandishi orodha ya miradi na shughuli iliyohuishwa ikioneshwa hali ya ulipaji wa Ada na Tozo za mwaka uliotangulia (2021/2022).

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira,
Makao Makuu, Kambarage, Ghorofa 6,
P. O. Box 2724,
Simu: +255 262960098, 0713608930,
Dodoma
Barua pepe: dg@nemc.or.tz
Tovuti: www.nemc.or.tz